# Madhara ya Janga la Korona
# KWA WANAWAKE
Wanaofanya **Biashara Rejareja** Katika Kaunti ya Mombasa

## MWONGOZO WA SERA


Photo courtesy Billy Miaron

**Njia na Namna ya Utafiti**

Janga la Korona limeathiri mazingira ya wafanyabiashara wote, na tofauti ilioko katika mfumo wa biashara na vizuizi huenda zikaleta athari za tofauti za kijinsia. Hata hivyo, nyingi ya sera za mwanzo hazijatumia vichujio vya kijinsia. Ili kuhakikisha kunapatikana utoshelezaji, kuanzia sasa kuendelea sera zitafaidi kutoka kwa uzingatifu wa jinsia moja, k.v kushughulikia jinsia zote.

Kuna aina nyingi za haiba tofauti za biashara zinazomilikiwa na wanawake na wanaume ambazo zinaathiri kuimarika kwao dhidi ya janga la KORONA.

Wanawake wana uwezekano mkubwa kufanya katika sekta za biashara zilizoathirika zaidi kwa kupoteza wateja ukilinganisha na wanaume (k.v. za rejareja, sekta ya mikahawa na utalii). Wanawake wana mgao mdogo sana wa malipo ya utunzaji katika majukumu yao, ambayo yameongezeka kutokana na amri ya kukaa nyumbani.

Matatizo haya yanaongezeka kwa kuzingatia kwamba kwa wastani biashara zinazomilikiwa na wanawake ni ndogo na chache. Kuna uwezekano kuwa zitafadhiiliwa na wao binafsi, au kufadhiliwa na rafiki na wanafamilia, na zina mali za pesa zilizo kidogo. Wanawake wana nafasi finyu za kupata ufadhili wa kifedha kutoka nje, na viwango vidogo vya fahamu za kifedha za biashara ndogondogo na ujasiri mdogo ukilinganisha na wanaume. Wafanyabiashara wa kike uweka idadi ndogo ya nambari za mawasiliano, kama vile kamati za ushauri au washauri wa kitaalam, ili kuwafaa jinsi ya kupenya katika janga hili. Wanawake wana uwezekano mdogo wa kutumia mitandao kupata suluhu ya kibiashara, ambayo itachangia uwezo wao kuingia katika biashara za mitandaoni. Tofauti hizo hazijaangaziwa kwenye mikakati ya kufaa biashara ndogondogo kutokana na KORONA. Wanaweka hawajafuzu katika mipango ya kuwafaa ambayo imeletwa kufika sasa – kwa sababu ya mifumo ya biashara zao, kushindwa kuafikia viwango hitajika vya mapato, au kutokuwa na mazoea ya kutumia mikopo ya kifedha ya benki, ambayo ni njia moja inayopendelewa ya kutumia mikopo ya kifedha ya benki, ambayo ni njia mojawapo inayopendelewa ya kutumia fedha za dharura za kusaidia mashirika madogomadogo.

# MIANYA ILIYOPO YA SERA

1. Kaunti ya Mombasa imekosa sera/sheria za Masoko na Biashara za kusaidia kuangazia mahitaji yalipo ya wafanyabiashara wa kike

2. Kaunti ya Mombasa bado haijaanza kutumia Mwongozo wa Utoaji wa huduma Muhimu za Afya wakati wa dharura

3. Pesa za Kuendeleza Wanawake (WEF) zinaangazia kwenye makundi ya kinamama hivyo basi kuwafungia wafanyabiashara wanawake wanaojisimamia binafsi kupata mikopo

4. Licha ya kujitolea idara ya Mikakati ya Kinga ya Kijamii ya Kaunti ya Mombasa (2018 – 2021) ya kuboresha bima ya afya kwa umma kutoka asilimia 26.7% hadi 60%, idadi kubwa ya wanawake katika biashara za rejereja hawajajisajili katita NHIF

5. Ikiwa sehemu ya mpango wa utekelezwaji wa Ruwaza ya 2030 katika kiwango cha kaunti, Serikali ilianzisha kituo cha *Biashara* cha Mikopo ya Biashara Ndogo na Wastani (MSME) mwaka 2021. Hata hivyo, wafanyabiashara wa kike hawajapata faida kuhusiana na mafunzo ya uzalishaji, uidhinishwaji wa bidhaa na mikopo

**Madhumuni ya Utafiti Huu**

Madhumuni ya utafiti huu ni pamoja na:

- Kuweka sera na mianya inayotumika katika kuimarisha na uwezeshaji wa wafanyabiashara wanawake katika kaunti ya Mombasa
- Kwa kutambua athari za kiuchumi na kijamii za janga la KORONA kwa wafanyabiashara wanawake katika Kaunti ya Mombasa
- Ili kutoa mapendekezo kwa wahusika ili kuchukua hatua zinazolenga kuimarisha wafanyabiashara wa kike katika kaunti ya Mombasa

**Mbinu na Eneo lengwa**

Shirika la Uhusishaji wa Wanawake katika Maendeleo lilitumia mbinu ya ukusanyaji data ya maelezo jumla na uchanganuzi. Taarifa msingi za kwanza zilitolewa kutoka kwa wajumbe wa idara za kaunti za afya, kilimo, biashara, jinsia, na vijana; mashirika ya kijamii yanafanya kazi ya kuwezesha wanawake kiuchumi na afya; na wanawake binafsi wenye biashara rejareja. Taarifa za pili zilipatikana kutoka katika dawati la uchunguzi wa sheria, sera, ripoti za utafiti, taarifa za serikali, ripoti na viacho vingine vya taarifa za mtandaoni. Utafiti huu uliangazia kaunti-ndogo za (Changamwe, Jomvu, Nyali na Kisauni) katika kaunti ya Mombasa. Taarifa kutoka kwa waliojibu maswali inawakilisha aliyopitia mtu binafsi na dhana na ripoti hii inaichukulia mitazamo hiyo jinsi ilivyo.

**Matokeo Muhimu**

Mahitaji ya chini, mauzo ya chini, na mapato ya chini: Kwa sababu ya KORONA kumekuwa na ukosefu na nafasi za kuleta mapato ambazo zilichangiwa na kusitishwa kwa shughuli za kimapato, wafanyabiashara wanawake wanaumia kiuchumi kutokana na bidhaa zao ambazo hazijauzwa na mara nyingi zimeharibika kwa sababu ya uasilia wake wa kuaharibika.

Biashara ndogo za rejareja ambazo bado zimefunguliwa hazifunguliwi wakati wote: hatua ya serikali ya kutekeleza magizo ya KORONA kama vile kafyiu ilididimiza biashara nyingi kama vile baa/maduka ya kuuza pombe kwa sababu muda wao wa kufanya kazi ulichukuliwa kuwa kinyume na sheria hivyo basi kusitisha shughuli za biashara. Hii pamoja na kupambana na muda huku kafyiu ikikaribia na kujazana katika mitaa/masoko ilisababisha hasara hasa kwa bidhaa za kilimo kama vile nyanya, mayai, mboga & samaki.

Hali mbaya ya madeni kwa wafanyabiashara inaendelea kuwakumba katika upataji wa mikopo wasambazaji, ambao pia wanahangaika kwa changamoto za kifedha, mauzo ya chini, na ukiukaji wa kulipa deni: Idadi inayoibuka ya biashara za wanawake (20%) iliripoti kupungua kwa uwepo wa mikopo kutoka kwa wasambazaji kuanzia Disemba 2020 hadi Mei 2021. Huku na wasambazaji nao kwenye uboreshaji wa bidhaa wakikumbana na ukosefu wa pesa kutokana na ukosefu wa ufadhili kutoka katika taasisi za kifedha, kupungua kwa mauzo, na kuongezeka kwa gharama, wamepunguza uuzaji kimikopo.

Upungufu wa Bima za afya: Wanawake katika biashara za rejareja hawana nafasi za kufikia huduma bora katika vituo vya afya vya umma na huduma ambazo mara nyingi zimejaa, hazitoshelezi, ghali, na mbali kutoka mahali pa kazi.

Suala kuu kwa wanawake wafanyabiashara wa rejareja ni nafasi ilipotezwa kwa muda unaotumiwa katika vituo vya afya ambavyo vimejaa na athari mbaya kweye mapato yao.

ambacho kimejaa, inamaanisha kwamba hawezi fanya kazi na atapoteza mapato. Wakati wa KORONA,

wafanyabiashara rejareja wa kike hawana nafasi nzuri ya kupata taarifa muhimu za KORONA na zile za kufikia huduma za afya.**Utunzaji wa bure na kazi za nyumbani:** Huku KORONA ikifanya kazi ya utunzaji kuonekana kuwa suala la kisera, bila shaka imepanua mwanya wa ukosefu wa usawa kijinsia na kiuchumi. Familia nyingi zimepata majukumu mengi ya kutunza wakati wa janga hili, na wanawake wabeba mzigo wa majukumu hayo ya utunzaji. Idadi kubwa ya wanawake wafanyabiashara ndogondogo Mombasa ni masikii na wanakaa katika makaazi duni; wao ni miongoni mwa waliotengwa katika jamii, wana nafasi finyu za kupata ajira rasmi za kulipwa, kinga ya kijamii, huduma za afya, na huduma za umma.

**Mapendekezo**

·Pesa ya matumizi ya Kaunti ya Mombasa na ile ya Maendeleo ya Wanawake sharti iwe na mipangilio ya kuwafundisha wafanyabiashara wa kike jinsi ya kupata mikopo.

·Idara ya Huduma za Afya katika Kaunti ya Mombasa inafaa kuharakisha kuanza kutumia Mwongozo wa Upatikanaji wa Huduma Muhimu, 2020.

·Idara ya Huduma za Afya katika Kaunti ya Mombasa inafaa kuharakisha kuanza kutumia Mwongozo wa Upatikanaji wa Huduma Muhimu, 2020.

·Wahusika katika mashirika ya kijamii, na mashirika mengine ya sekta za kibinafsi pamoja na miungano kama vile Shirika La Kitaifa Kibishara (KNNCI) yanafaa kuongeza huduma za ushauri na Nasaha kwa wafanyabiashara wa kike. Hii injumuisha ushauri wa jinsi ya kuimarisha biashara ambazo zimeathirika na kuwainua ili kusimamisha biashara zao.

·Kaunti ya Mombasa inafaa kuanzisha sera/sheria za Masoko na Biashara ili kufaa mahitaji ya zaidi ya mabanda 500 ya masoko na nafasi ilivyodhamiriwa katka Kinga ya Kijamii ya Kaunti.

·Idara ya Uangalizi na Uhakiki, pamoja na utafiti ya Kaunti inafaa kuanza taarifa za kijinsia za kuangalia athari za KORONA na mpango wa kusaidia ushiriki wa biashara na matokeo.

## Hitimisho

MSMEs imesadia sana katika ukuaji wa kiuchumi nchini Kenya. Sekta hii kwa ukubwa inajumuisha biashara ndogondogo na inachangia takribani 40% kwa uchumi wa nyumbani GDP. MSMEs imeajiri watu milioni 14.9, ambapo watu milioni 12.1 wameajiriwa kwenye biashara ndogondogo. Hata hivyo, sekta hiyo bado imebaki kuwa ya rejareja kwani ni 20% tu kwa watu milioni 7.4 wa MSMEs ambao hufanya shughuli zao wakiwa wameidhinishwa kwa kupewa leseni. KORONA imekuwa na athari mbaya kwenye uchumi kwa jumla. Biashara nyingi zimefungwa na wengi wa watu kupoteza kazi. Kwa sababu hiyo, uwezo wa wateja wa kununua haupo. Wanunuzi wanatumia mda mfupi kwa matumizi ya pesa yasiyo ya lazima na kuangazia bidhaa muhimu pekee. Huku uchumi ukianza kufunguka polepole na masharti yamepungua, na watumiaji bidhaa wanaogopa na wamekuwa wakitumia pesa kwa makini na hivyo kuwalemea wafanyabiasha wa kike wa rejareja.

.